# II.
# Usimamizi wa stoo

## Mada ya 29a

# Kwa nini vyombo vitupu vya pembejeo visitumiwe tena

IFDC

# JARIDA LA UHAKIKA


## II. Usimamizi wa stoo

## <u>Mada ya 29a:</u> Kwa nini vyombo vitupu vya pembejeo visitumiwe tena

Pembejeo za kilimo zinazouzwa sokoni kwa wakati wote huwekwa kwenye vyombo, masanduku, au mifuko iliotengenezwa kutoka kwa nyenzo tofauti. Katika bara la Afrika, ni kawaida kuona vyombo hivi **vikitumiwa tena** kubeba maji, chakula, n.k. baada ya kutolewa pembejeo za kilimo.

Hata hivyo, ni **HATARI** sana kutumia tena chombo chochote cha pembejeo za kilimo. Hata pakiti hizi zikisafishwa, bado kuna **mabaki** ndani yake ambayo **hayawezi kuonekana** kwa macho yasiosaidiwa. Ingawa chombo/pakiti inaonekana safi na tupu, haki ni kwamba sio hivyo.

Vyombo vitupu au pakiti zikitumiwa, mabaki **hukwamilia au huchanganyika na** bidhaa zilizobebwa ndani yake. Wakati tu binadamu anashika au anala maji au chakula, **anaathiriwa** na mabaki na atapata dalili kama za mtu aliyeathiriwa na pembejeo za kilimo.



Mtu anaathiriwa au kuchafuliwa na mabaki

**KWA HIVYO, VYOMBO VITUPU VISIWAHI KUTUMIWA TENA!**

Mifano michache ya vile watu wanaweza kuchafuliwa/kathiriwa kwa kutumia tena vyombo vitupu vya pembejeo za kilimo:

- Mkulima anatumia tena mfuko mtupu wa mbolea **kusafirishia** kakao yake hadi mahali pa kununua. Baada ya uchanganuzi, inapatikana kwamba kakao imechafuliwa na mbolea. Kakao hiyo inaharibiwa na mkulima halipwi kwa kakao yake.
- Kijana mdogo anatengeneza **kidude cha kuchezea** kwa kutumia chombo kitupu cha viuawadudu kilichosuuzwa mara tatu. Anashika kidude hicho anapocheza na kukimbizwa hospitali kwa sababu alipata vipele kwa mkono.
- Mwanamke anatumia tena chombo kitupu cha viuawadudu **kubebea maji** kutoka kwa kisima hadi nyumbani. Familia yote inakunywa maji na inakimbizwa hospitalini kwa sababu ya uchafuzi/kuathiriwa.

# MWONGOZO

## II. Usimamizi wa stoo

## Mada ya 29a: Kwa nini vyombo vitupu vya pembejeo visitumiwe tena

**Vifaa vinavyohitajika:**

- ☑ Ubao ulio na makaratasi
- ☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)

**Muda unaohitajika:** Dakiki 30

**Maandalizi:**

- ☑ Makaratasi ya kufungua kurasa yalio na kichwa: *Kwa nini vyombo vitupu vya pembejeo visitumiwe tena*
- ☑ Chupa ya maji ilio tupu
- ☑ Chupa ilio na kitu kama majimaji lakini kizito na cha kukwamilia kama mafuta ya mnazi
- ☑ Chupa iliokamuliwa na ilio na kitu kama maji lakini nzito na cha kukwamilia ili uweze kuona mabaki.

## Mwanzo

**U**sikivu: Waonyeshe chupa tupu ya maji. Waambie kwamba hii chupa ilikuwa na kitu majimaji lakini umeisafisha. Waulize: “Hi chupa ni tupu?” Wacha watu wachache wajibu, lakini usitoe maoni yako.

**K**ichwa: Waambie kichwa: *Kwa nini vyombo vitupu vya pembejeo visitumiwe tena.*

**K**usadikika/: Elezea uzoefu wako na pembejeo za kilimo.

**M**alengo: Kueleza ni kwa nini vyombo vitupu visitumiwe tena na kuonyesha matokeo/madhara zinapotumiwa tena.

**M**anufaa: Kutumia tena vyombo vitupu vya pembejeo za kilimo kunaweza kuleta hatari kubwa sana kwa afya na mazingira.

Kujua kwa nini vyombo hivi visitumiwe tena kutakusaidia kuepuka ajali nyingi na uchafuzi.

**M**welekeo: Katika kipindi hiki, hatutajadili jinsi ya kutupa vyombo vitupu.

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Waonyeshe chupa tupu na uwaambie kwamba wale waliosema kuwa haikuwa tupu walisema ukweli. Ingawa chupa inaonekana tupu kwa macho, ina **mabaki** ndani.
2. Waambie kwamba **utawaonyesha** mabaki. Waonyeshe ile chupa ilio na majimaji nzito nay a kukwamilia. Waambie kwamba katika kipindi kijacho, tutajifunza jinsi ya kusafisha vyombo vitupu na kufafanua mbinu ya kusuuza mara tatu. Kusuuza mara tatu kunamaanisha unamwaga majimaji yote yalio chupani na kuisuuza mara tatu ukitumia maji masafi.
3. Waonyeshe chupa tupu iliokuwa na majimaji nzito na ya kukwamilia na uwaambie kwamba chupa hii ilisuuzwa mara tatu na maji masafi. Waulize kama chupa ni **safi.** Watasema: hapana. Waulize kwa nini? Watasema kwamba kuna majimaji kidogo iliokwamilia ndani mwa chupa.
4. Waonyeshe **chupa tupu tena**. Waambie kwamba chupa hii pia ilikuwa na majimaji na ilisuuzwa mara tatu. Uliza tena kama chupa ni tupu. Unatarajia watasema; hapana. Jifanye umeshituka na uwaulize: “Lakini hakuna kitu ndani. Siwezi kuona majimaji yote iliosalia.” Unatarajia mtu atasema kwamba ingawa huoni chochote, kuna mabaki ndani yake. Mpongeze mtu huyo kwa jibu lake sahihi na ukariri kwamba chupa hii **inaonekana** tupu lakini sio tupu. Hata kama imesuuzwa mara tatu, kuna **mabaki** ambayo hayawezi kuonekana na macho.
5. Waambie kwamba watu kwa jumla **hawajui** kama chupa tupu bado zina mabaki. Waulize kama washaona watu wakitumia tena vyombo vitupu vya pembejeo za kilimo. Waulize wapeane mifano ya vile vyombo hivi hutumiwa tena. Peana mifano kutoka kwa uzoefu wako pia. Orodhesha mifano kwa karatasi.
6. Uliza mifano ya vile mtu aua mazingira inaweza **kuchafuliwa**. Sisitiza kwamba uchafuzi unaweza kutokea hata kama chombo kimesafishwa. Pia sisitiza kwamba hatuwezi kuona mabaki na macho lakini yako ndani.

# Malizia

**M**uhtasari: Toa muhtasari kwa kuwaambia kwamba vyombo vitupu vya pembejeo za kilimo visiwahi kutumiwa. Hata ikisafishwa sana, kuna mabaki ambayo hayawezi kuonekana na yanaweza kulsababisha uchafuzi.

**M**aswali: Uliza kama kuna yeyote aliye na swali au maoni.

**T**athmini: Waulize kueleza kwa tusiwahi kutumia tena vyombo vitupu vya pembejeo za kilimo.

**H**atua fuatilizi: Katika kipindi hiki, tumeona kwa nini hatufai kutumia tena vyombo vitupu vya pembejeo za kilimo. Katika kipindi kifuatacho tutajadili jinsi ya kusafisha na kutupa vyombo vuitupu ili visitumiwe tena.

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.